

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آتَيْنَا مِنْكُمْ وَعَجِلُوا الظَّلَمَ لِيَسْتَغْنُوكُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَغْنَى
الَّذِينَ مِنْ قَلْبِهِمْ وَلَيُسْكِنَنَّ لَهُمْ دِيْنُهُمُ الَّذِي أَرْفَعْنَا مِنْهُمْ وَلَيُبَشِّرَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَهُمْ أَنَّهُ
يَعْبُدُونِي لَا يُشْكُونَ فِي شَيْءٍ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّافِرُونَ

Na: 05 / 1446 H

Ijumaa, 20 Jumada I 1446 H

22/11/2024 M



Taarifa kwa Vyombo vyta Habari

Uvamizi Mpya wa Hay'at Tahrir al-Sham kwa Wanachama wa Hizb ut Tahrir: Hatua ya Kuelekea Uhalalisha Mahusiano au Kuelekea Kujisalimisha?! (Imetafsiriwa)

Uvamizi mpya wa Huduma ya Kuu ya Usalama yene uhusiano na Hay'at Tahrir al-Sham (HTS) kwa wanachama wa Hizb ut Tahrir uliku baada ya jina kupendekezwa kwa Ijumaa ya 22/11/2024: "Yeyote Anayelinda Mipaka ya NATO, Kuzuia Ufunguzi wa Vita na Kulinda Mipaka ya Utawala." Huduma Kuu ya Usalama, baada ya uhamasishaji mkubwa iliyoufanya mnamo Ijumaa usiku, iliteka nyara idadi mpya ya wanachama wa Hizb ut Tahrir, ambao ni wakili Muhammad al-Sharif na Fateh al-Tarmanini kutoka mji wa Tarmanin, pamoja na mwanachama Omar Rahhal kutoka mji wa Kafr Nouran, na ndugu wawili, wanafunzi Bashar Abdul-Hay Samsoum na Ahmad Abdul-Hay Samsoum kutoka mji wa Atarib. Hapo awali, Sheikh Amir Salim, ambaye alihamishwa kutoka Jimbo la Daraa, alitekwa nyara.

Jina la Ijumaa hii liliku baada ya matamshi ya Ahmad Zidan ambapo alitaja kuwa Hay'at ilikuwa na dori kubwa katika kulinda mipaka ya NATO kwa kulinda mipaka ya Uturuki, mwanachama wa muungano huo, ambao ulisababisha hali ya chuki ya wananchi eneo hilo kwa wanamapinduzi, hasa Mujahidina.

Maneno ya Zidan ndani yao yalibeba kisu cha wazi kwa Mujahidina, ambacho ni kisingizio ambacho Hay'at imekuwa ikitumia kuwadunga wale wanaopinga sera na fikra zake. Hivyo inadhihirika kutokana na maneno ya Zidan nani anawachoma kisu Mujahidina kwani Zidan katika kauli yake aliwaweka Mujahidina katika nafasi ya walini wa mipaka ya NATO na kuwafanya watekelezaji wa ajenda za nchi za Magharibi zinazo kula njama dhidi ya mapinduzi ya Ash-Sham, na anajua kwa yakini kwamba Mujahidina wa mapinduzi ya Ash-Sham hawakutoka ila kwa ajili ya jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu na kupindua utawala wa kihalifu jijini Damascus.

Enyi Watu wetu katika Mapinduzi ya Ash-Sham, Enyi Mujahidina: Mnaona kila siku, kwa macho yenu wenyewe, jinsi uongozi wa Hay'at na wananaadharia wake wanavyowaona nyinyi. Hawakuchukuliini chochote isipokuwa zana wanazotumia kutekeleza ajenda walizopangiwa ili kukomesha jihad yenu, mapinduzi yenu na kujitolea kwenu. Kwa hiyo, mutafanya nini?!

Enyi Mujahidina: Uongozi wa Hay'at na wananaadharia wake wanakuuhujumuni na matendo yenu kwa ufidhuli, na wanafanya kazi ya kukuzuieni kuwazunguka wale wanaofanya kazi ya kukulinden, jihad yenu, na mihanga yenu.

Leo, mapinduzi yanapita kwenye njia panda hatari. Ima mubakie kwenye njia ya uongozi wa Khay'at na viongozi wanaoshirikiana nao, na hivyo watekeleze kuitia nyinyi mipango na njama za nchi wanazozisuka wakati wa makongamano yao, au mumtegemee Mola wenu na mushikamane na kamba ya Mwenyezi Mungu peke yake, na mushikamane na misimamo ya mapinduzi yenu, na muendelee na uongofu na ufahamu pamoja na kiota chenu cha mapinduzi na watu wenu ambao wana shauku kwenu kufikia matunda ya jihad yenu kupindua utawala wa kihalifu nyumbani kwake, Damascus, na kusimamisha utawala wa Uislamu juu ya magofu yake.

Enyi Mujahidina: Jueni kwamba nyinyi ndio tumaini la watu wenu na kiota chenu. Hakika historia inarekodi misimamo, basi chagueni misimamo ya heshima kwa ajili yenu, watu wenu, kiota chenu, na Ummah wenu unaotamani kuwa nanyi mpaka Mwenyezi Mungu Atukirimu sote kwa ushindi na tamkini. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[إِنَّمَا يَأْيُهُ الَّذِينَ آتَيْنَا إِسْتَجْبَيْوْا لِلَّهِ وَلِرَسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحِبِّيْكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ]

"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa." [Al-Anfal: 24].

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Syria